FUNZO LA 19

1. Je, watu waliozaliwa baada ya Nuhu ni nani?
-Hao walikuwa mababu wako na mababu wangu.

2. Je, mababu wetu walijua kuhusu Mungu?
-Ndiyo.

3. Je, mababu wetu walijuaje kuhusu Mungu?
-Kwanza, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kwa sababu wazee waliwaambia watoto habari za Mungu na mafuriko.

4. Je, wazee waliwaambia nini watoto kuhusu Mungu na mafuriko?
-Wazee waliwaambia watoto kuwa Mungu anachukia dhambi, na hivyo basi, aliwaharibu watu wote isipokuwa Nuhu na jamii yake.

5. Je, mababu wetu walijuaje tena kuhusu Mungu?
-Pili, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kupitia upinde wa mvua.

6. Je, upinde wa mvua uliwaambia nini mababu wetu kuhusu Mungu?
-Ya kuwa Mungu anawapenda watu, na kuwa hatawaangamiza watu tena kwa gharika.

7. Je, mababu wetu walijuaje tena kuhusu Mungu?
-Tatu, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kwa sababu anga, milima, mito, na miti iliwaambia kuhusu Mungu.



8. Je, anga, milima, mito, na miti iliwaambia nini mababu wetu kuhusu Mungu?
-Ya kuwa Mungu pekee ni Mungu, na kwambu watu wamfuate Mungu pekee.

9. Ijapokuwa mababu wetu walijua kuhusu Mungu, je, wengi wao walimwamini Mungu?
-La.
-Ni wachache kati ya mababu wetu waliomwamini Mungu.

10. Badala ya kumfuata Mungu, wengi wa mababu wetu walimfuata nani?
-Wengi wa mababu wetu walimfuata Shetani na uongo wake.

11. Je, Shetani aliwaambia mababu wetu wafanye nini?
-Waabudu jua, mwezi na nyota.
-Waabudu maroho.
-Waabudu sanamu za mbao na mawe zinazofanana na watu na wanyama.

12. Je, ni kwa nini Mungu hakutaka watu wote waishi katika sehemu moja duniani?
-Ili wasimsahau Mungu na dhambi zao ziwe nyingi sana.

13. Je, ni kwa nini watu waliaza kujenga mnara mrefu Babeli?
-Kwa sababu watu walikuwa na kiburi sana.
-Kwa sababu watu walitaka kujifanyia jina wenyewe.

14. Je, watu walipoanza kujenga mnara, Mungu aliona?
-Ndiyo.

15. Je, Mungu anayajua mawazo ya watu?
-Ndiyo.
-Kabla hata mtu kuanza kuwaza, Mungu anayajua mawazo ya huyo mtu hadi mwisho.

16. Je, Mungu anayajua maneno yote ya watu wote?
-Ndiyo.
-Kabla ya mtu kuanza kusema neno, Mungu anayajua maneno yake yote.

17. Je, Mungu anayajua maneno yote ya watu wote?
-Ndiyo.
-Kabla hata mtu kuanza kusema neno, Mungu anayajua maneno yake hadi mwisho.

18. Je, Mungu huwasahau watu?
-Mungu hasahau mawazo ya watu.
-Mungu hasahau wanachosema watu.
-Mungu hasahau wanachofanya watu.

19. Kwa sababu mababu wetu hawakumtii Mungu, Mungu aliamua kuwaadhibu, Je, ni adhabu gani ambayo Mungu angewapa?
-Mungu angewapa lugha tofauti ili wasielewane.

20. Baada ya Mungu kuwapa watu wote lugha tofauti, Je, Mungu alifanya nini tena?
-Mungu aliwatawanya watu wote katika sehemu tofauti duniani.



21. Je, mababu wako walifika vipi huku?
-Baada ya miaka mingi sana, mababu wako walikuja hapa kwa miguu na kwa mashua.

-Mababu wetu walioishi baada Nuhu hawakumtii Mungu, na wakajenga mnara wa Babeli.

-Walifuata uongo wa Shetani wala si ukweli wa Mungu.

-Walifuata njia yao na wakamkataa Mungu.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Je, mungu aliacha mpango wake wa kuwaokoa?
-La.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Je, Mungu aliacha mpango wake wa kutuma Mwokozi?
-La.

-Ikiwa Mungu ataahidi, lazima atamize.

-Katika Bustani ya Edeni, Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi.

-Mungu hawezi vunja ahadi yake.

-Mungu aliwaahidi Sethi, Enoko na Nuhu kwamba angetuma Mwokozi.

-Mungu hawezi vunja ahadi yake.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu hakuwacha mpango wake wa kutuma Mwokozi.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu bado alitaka kutuma Mwokozi ili awaokoe watu kutokana na dhambi.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu bado alitaka kutuma Mwokozi ili awaokoe watu kutokana na kifo.

-Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu bado alitaka kutuma Mwokozi ili awaokoe watu kutokana na Shetani.

-Je, watu waweza kumzuia Mungu kutuma Mwokozi?
-La.

-Je, mapepo waweza kumzuia Mungu kutuma Mwokozi?
-La.

-Je, Shetani anaweza kumzuia Mungu kutuma Mwokozi?
-La.

-Ni nani anaweza kumzuia Mungu kutuma Mwokozi?
-Hakuna yeyote.

-Mungu alipoamua kutuma Mwokozi, hakuna anayeweza kumzuia kutuma Mwokozi.

-Kwa sababu mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu aliamua kumchagua mtu mmoja ambaye kupitia kwake Mungu angemtuma mwokozi.



-Jina la mtu huyo ni Abramu.

-Mungu aliamua kutuma mwokozi kupitia kwa Abramu.

-Je, kwa nini Mungu alichagua Abramu ambaye Mwokozi alikuja kupitia kwake?

-Je, Mungu alimchagua Abramu kwa sababu Abramu hakutenda dhambi?
-La.

-Abramu alikuwa mwenye dhambi.

-Abramu alikuwa kizazi cha Adamu.

-Abramu alizaliwa katika dhambi.

-Je, ni kwa nini Mungu alimchagua Abramu?

-Abramu aliamini kuwa Mungu ni mtakatifu.

-Abramu aliamini kwamba alikuwa amtenda dhambi.

-Abramu aliamini kuwa dhambi yake ilistahili kifo.

-Abramu aliamini kuwa ni Mungu pekee ambaye alikuwa na uwezo wa kumwokoa.

-Abramu aliamini kuwa Mungu angemtuma Mwokozi.

-Kwa sababu Abramu aliamini Mungu, Mungu alichagua kutuma Mwokozi kupitia kwa Abramu.

-Baba ya Abramu alikuwa ni Tera.

-Tera alikuwa ni kizazi cha Shemu.

-Je, unakumbuka majina ya wana wa Nuhu?

-Shemu, Hamu na Yafethi.

-Abramu alikuwa kizazi cha Shemu, mmoja wa wana wa Nuhu.

Tusome Mwanzo 11:27 & 29-30

27-Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu.
29-Abramu na Nahori wakajitwalia wake. Jina la mkewe Abramu aliitwa Sarai, na jina la mkewe Nahori aliitwa Milka, binti Harani, ambaye alikuwa baba wa Milka na wa Iska.
30-Na Sarai alikuwa tasa, hakuwa na mtoto.

-Siku moja, Abramu alioa.

-Abramu alimuoa mwanamke anayeitwa Sarai.

-Lakini, Abramu na Sarai hawakuwa na mtoto.

-Je, ni kwa nini Abramu na Sarai hawakuwa na watoto?



-Kwa sababu Sarai alikuwa tasa.

-Abramu na Sarai waliishi katika mji wa Uru.

-Watu wa Uru hawakumwamini Mungu na kweli zake.

-Watu wa Uru walimfuata Shetani na uongo wake.

-Watu wa Uru walikuwa waovu.

-Abramu alipokuwa akiishi Uru, Mungu alimtokea Abramu.

-Hivi ndivyo Mungu alimwambia Abramu:

Tusome Mwanzo 12:1

1-Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha;

-Je, Mungu alimwambia Abramu afanye nini?

-Mungu alimwambia Abramu atoke katika nchi yake na aende katika nchi ambayo Mungu angemwongoza.

-Je, ni kwa nini Mungu alimwambia Abramu atoke Uru na nchi yake?

-Kwa sababu watu wa Uru hawakumwamini Mungu na kweli zake.

-Kwa sababu watu wa Uru walimfuata Shetani na uongo wake.

-Kwa sababu Mungu alitaka kujitengea watu ambao wangemwamini Mungu.

-Je, Mungu alinena vipi na Abramu?

-Mungu alinena na Abramu kupitia sauti yake.

-Mungu alinena na Abramu kwa sauti yake kwa sababu Biblia yake haikuwa bado imeandikwa.

-Je, Mungu hunena vipi na sisi siku hizi?

-Siku hizi, Mungu mara nyingi haneni nasi kupitia kwa sauti yake.

-Siku hizi, Mungu hunena nasi kupitia kwa Neno lake, Biblia yake.

-Twaweza kusikia maneno yake kwa kuyasoma katika Biblia.

-Twaweza kujua anachotuambia Mungu kwa kusoma maneno yake katika Biblia.

-Mungu aliponena na Abramu, alimuahidi kitu.

-Kifuatacho ndicho alichomuahidi Abramu:

Tusome Mwanzo 12:2



2-Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka;

-Je, Mungu alimuahidi nini Abramu?

-Kwanza, Mungu alimuahidi kuwa uzao wake utakuwa mwingi na pia watakuwa watu wakuu.

-Wakati huo, Abramu na Sarai walikuwa na watoto wangapi?
-Hakuna.

-Je, ni kwa nini Abramu na Sarai hawakuwa na watoto?

-Kwa sababu mke wa Abramu, Sarai, alikuwa tasa.

-Ingawaje Abramu hakuwa na watoto, Mungu alimuahidi Abramu kuwa uzao wake ungekuwa mwingi.

-Pili, Mungu aliahidi kuwa atambariki.

-Tusome kile Mungu alimuahidi Abramu tena:

Tusome Mwanzo 12:3

3-Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.

-Tatu, Mungu alimuahidi kuwa atawabariki wale watakao mbariki, na kuwalaani wale watakao mlaani.

-Nne, Mungu aliahidi kuwabariki watu wote kupitia kwa mmoja wa uzao wa Abramu.

-Hii ahadi ya kuwa Mungu atawabariki watu wote kupitia kwa mmoja wa uzao wa Abramu ndiyo ahadi kuu zaidi.

-Je, ni nani huyo katika uzao wa Abramu ambaye kupitia kwake watu wote wangebarikiwa?

-Mwokozi.

-Mwokozi angefanya nini?

-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu za dhambi.
-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu za kifo.

-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu Shetani.

-Mwokozi angekuja kuwapatanisha watu na Mungu tena.

-Mwokozi angemshinda Shetani na kuwabariki watu wote ulimwenguni.

-Je, Abramu aliamini ahadi za Mungu?
-Ndiyo.

-Abramu aliamini kuwa Mungu hawezi danganya.

-Abramu aliamini kuwa Mungu hunena kweli pekee.



-Baada ya Mungu kumuahidi Abramu, Abramu alifanya nini?

Tusome Mwanzo 12:4-5

4-Basi Abramu akaenda, kama Bwana alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abramu alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani..

5-Abramu akamchukua Sarai mkewe, na Lutu mwana wa nduguye, na vitu vyao vyote walivyokuwa wamejipatia na hao watu waliowapata huko Harani, wakatoka ili kwenda nchi ya Kanaani; nao wakaingia katika nchi ya Kanaani.

-Abramu alitoka katika nchi aliokuwa akiishi, na akamfuata Mungu kuelekea nchi aliokuwa akimwelekeza.

-Je, Mungu alimwelekeza Abramu wapi?

-Mungu alimwelekeza Abramu kwa nchi iitwayo Kanani.

-Katika fundisho linalofuata, tutajifundisha kilichomfanyikia Abramu katika nchi ya Kanani.